TAARIFA HALISI NAMBA TISA

"WANAWAKE NA WASICHANA: WANAATHIRIKA ZAIDI, LAKINI WANAPATA HUDUMA DUNI"

Wanawake ni asilimia 53 ya watu wote wanaoishi na VVU barani Afrika na mwaka 2005 takwimu zilionyesha kuwa asilimia 77 ya wanawake wote wanaoishi na VVU duniani kote wako katika nchi za Afrika, kusini mwa Jangwa la Sahara:

Afrika ni kanda pekee duniani ambayo wanawake walioambukizwa virusi ni wengi kuliko wanaume. Takwimu hizo zinaonyesha kwa kila wanaume 10 walioambukizwa, wanawake 13 wana VVU.

Nafasi isiyo sawa ya wanawake katika jamii nyingi, viwango vikubwa vya unyanyapaa kingono, ugomvi na unyanyasaji, na hatari zaidi ya wanawake kuambukizwa VVU, vyote vinachangia katika kuufanya ugonjwa uwe wa **"wanawake zaidi".**

Mzigo mkubwa wa VVU/UKIMWI unawaangukia hasa wanawake katika nchi za Afrika, kusini mwa Jangwa la Sahara, kama takwimu zinavyoonyesha hapo juu, na kutokuwa na usawa wa jinsia ni kipengele muhimu katika kuenea kwa ugonjwa. Maadili ya jamii na imani na mfumo dume wa kitabaka katika jamii vinadumisha hadhi ya chini ya wanawake, na kuwafanya wakose uwezo wa kujikinga na maambukizi wao wenyewe.

Wanakosa uwezo wa kujadiliana kuhusu ngono salama na kudhibiti ushambuliaji/ulazimishaji wa ngono.

- Asilimia 29 ya vijana walio katika umri wa balehe nchini Ghana waliofanyiwa utafiti mwaka 1999 wamesema kuwa uzoefu wao wa kwanza wa ngono ulitokana na kulazimishwa.

Wavulana na wanaume wanapokataa kutumia kondomu, wasichana na wanawake hawana uwezo wa kusisitiza. Kama kawaida, wasichana na watoto wanaendelea kubakwa siku hadi siku. Dhana ya thamani ndogo ya watoto wa kike ni sababu mojawapo, ingawa kuna imani kwamba kufanya ngono na msichana bikira ni tiba ya VVU. Wanaume pia wanawabaka wasichana kwa kudhani kwamba kwa kuwa ni vijana, basi hawana VVU.

- Nchini Zimbabwe kuna Asasi Isiyo ya Serikali iliyorekodi zaidi ya matukio 4,000 ya unyanyasaji wa kijinsia dhidi ya watoto katika sehemu moja tu ya nchi mwaka 2005.
- Mwanzoni mwa mwaka 2006 mkuu wa shule ya msingi nchini Zimbabwe alishitakiwa kwa kuwabaka wasichana sita.

Watu wazima wanaume ambao katika nchi nyingi wanajulikana kuwa "mabuzi" wanafanya ngono na wasichana wadogo kwa kuwapa chakula, nguo au vitu vya "anasa" kama vile simu za mkononi n.k.

- Utafiti uliofanywa Afrika Kusini umegundua kwamba wasichana wanaofanya ngono na wanaume wenye umri wa miaka mitano au zaidi kuliko wao wenyewe, wana uwezekano wa kupata VVU mara nne zaidi kuliko wale wenye wenzi wanaokaribiana nao ki-umri.

- Kwa Zulu – Natal, jimbo lenye maambukizi zaidi ya VVU Afrika Kusini, wanaume kutoka mji wa Vulindlela wanafanya kazi kama wahamaji na kurudi kila mwisho wa wiki, na kuwapa wasichana fedha kwa madhumuni ya kufanya nao ngono: Zaidi ya asilimia 25 ya wasichana wa Vulindlela kwa sasa wana VVU; zaidi ya asilimia 50 ya wanawake Vijana wenye umri wa miaka 20-24 wameambukizwa VVU, na kati ya asilimia 66 ya wanawake wenye umri wa miaka 25-29 pia wana Virusi Vya UKIMWI.

Wanaume wanaufanya ugonjwa huu kuwa wa wanawake wakati wanapokataa kupimwa VVU na halafu kuambukiza Virusi wake zao (mitara huchangia wake wengi wanaweza kuambukizwa) na kwa wapenzi wao.

- Wanawake wengi wanasema kwamba waume wao wanakataa kupimwa VVU au kutibiwa.
- Wengine wanasema kuwa waume wao wanawapiga na kuwafukuza nyumbani kwao iwapo watakuwa na VVU au kuonyesha dalili za maradhi hayo.
- Utafiti uliofanyika Afrika Kusini na Tanzania Umegundua kwamba wanawake waliopigwa na waume zao ni asilimia 48 wenye uwezekano wa kuambukizwa VVU kuliko wale ambao hawakupigwa.

Hitimisho

Uzuiaji wa VVU/UKIMWI miongoni mwa wanawake na wasichana unategemea kuwapa uwezo wa kujilinda wenyewe.

Unajumuisha kubadili mawazo, imani na desturi. Inahitajika kuwekwa na kufuatilia utekelezaji wa sheria kali za kuzuia ubakaji, unyanyasaji wa kijinsia na aina nyingine za ugomvi wa kijinsia. Utahitaji ushiriki wa kikamilifu na uhusishaji wa watu wote – hasa wanaume kama wenza katika vipengele vyote vya mabadiliko pamoja na viongozi wa jadi na dini, ili kubadili maadili ya kimila na desturi zinazowanyima uwezo wanawake.

- Nchini Zimbabwe, Serikali na Asasi Zisizo za Serikali zimeshirikiana katika kampeni ya "Kutovumilia unyanyasaji kwa watoto" inayowaelimisha jamii kuhusu kuwalinda wasichana dhidi ya ubakaji na unyanyasaji.

- Asasi Zisizo za Serikali nchini Afrika Kusini zimeanzisha kampeni ya **"Wanaume Halisi Hawabaki"** Mwanzoni mwa mwaka 2006 kushughulikia tatizo kubwa la ugomvi wa kijinsia nchini.
- Juhudi za kijamii nchini Swaziland zinategemea watu wazima wa kujitolea kama tegemeo la watoto, wanaotoa taarifa za matukio au vitisho vya unyanyasaji kwa mhusika, ambaye naye huwasiliana na mamlaka ya polisi.
- Ghana imeanzisha kikosi maalumu cha polisi cha **kuchunguza makosa ya ngono.**

Wanawake pia ni wanafamilia wanaowatunza wagonjwa na wanaofariki kwa UKIMWI.

- Iwapo wanakosa maarifa kuhusu maambukizo ya VVU, wataambukizwa kwa njia ya majimaji ya mwili wakati wa kuwatunza, au wakati wa matayarisho ya mwili kwa ajili ya mazishi, hasa katika jamii za kiasili za vijijini.

TAARIFA HALISI NAMBA TISA

- Mahitaji yanayohusu matunzo pia yanaathiri juhudi za wanawake za kujitafutia kipato, na kuwafanya wawe masikini zaidi na kuongeza uwezekano wa wao kudhulumiwa baada ya vifo vya wenzi wao.

Mkabala wa jumla wa kupunguza kasi ya maambukizi ya VVU unahitaji umakini zaidi katika masuala ya ugomvi wa kijinsia na ukosefu wa usawa wa jinsia katika jamii za Kiafrika. Wanawake na Wasichana wanahitaji:

- Taarifa sahihi na za kutosha kuhusu namna VVU vinavyoambukizwa na kuzuiwa.
- Uhimizaji wa sheria na sera zinazolaani na kuadhibu ugomvi wa kijinsia.
- Kuwasaidia wanawake kupata stadi wanazohitaji kujadiliana na wapenzi wao kuhusu matumizi ya Kondomu na upimaji na VVU na matibabu.
- Kujengwa kwa mazingira yatakayosaidia familia na jamii ambapo wanaume watashiriki kikamilifu katika kukomesha ubaguzi na ugomvi wa kijinsia na ambapo wasichana wanaweza kujenga utu, heshima na kujiamini ili waweze kujitetea dhidi ya maambukizi ya VVU.